# Hos

## Chapter 11

Swahili Interlinear

Reference: Swahili Biblica Neno

1

| Hebrew | Swahili | Strong's |
|---|---|---|
| כִּי | wakati | |
| נַעַר | mtoto | H5288 |
| יִשְׂרָאֵל | Israeli | H3478 |
| וָאֹהֲבֵהוּ | na-nilimpenda | H0157 |
| וּמִמִּצְרַיִם | na-kutoka-Misri | H4714 |
| קָרָאתִי | nilimwita | H7121 |
| לִבְנִי׃ | mwana-wangu | |

“Wakati Israeli alipokuwa mtoto, nilimpenda, nilimwita mwanangu kutoka Misri.

2

| Hebrew | Swahili | Strong's |
|---|---|---|
| קָרְאוּ | waliwaita | H7121 |
| לָהֶם | wao | |
| כֵּן | hivyo | |
| הָלְכוּ | waliondoka | H1980 |
| מִפְּנֵיהֶם | kutoka-kwao | H6440 |
| לַבְּעָלִים | kwa-Mabaali | |
| יְזַבֵּחוּ | walidhabihu | H2076 |
| וְלַפְּסִלִים | na-kwa-sanamu-za-kuchonga | H6456 |
| יְקַטֵּרוּן׃ | walifukiza | |

Lakini kadiri nilivyomwita Israeli, ndivyo walivyokwenda mbali nami. Walitoa dhabihu kwa Mabaali na kufukiza uvumba kwa vinyago.

3

| Hebrew | Swahili | Strong's |
|---|---|---|
| וְאָנֹכִי | na-mimi | H0595 |
| תִרְגַּלְתִּי | niliwafundisha-kutembea | H8637 |
| לְאֶפְרַיִם | Efraimu | H0669 |
| קָחָם | niliwachukua | H3947 |
| עַל־ | juu-ya | |
| זְרוֹעֹתָיו | mikono-yao | H2220 |
| וְלֹא | na-hawaku | H3808 |
| יָדְעוּ | jua | H3045 |
| כִּי | kwamba | |
| רְפָאתִים׃ | niliwaponya | H7495 |

Mimi ndiye niliyemfundisha Efraimu kutembea, nikiwashika mikono; lakini hawakutambua kuwa ni mimi niliyewaponya.

4

| Hebrew | Swahili | Strong's |
|---|---|---|
| בְּחַבְלֵי | kwa-kamba-za | |
| אָדָם | binadamu | H0120 |
| אֶמְשְׁכֵם | niliwavuta | H4900 |
| בַּעֲבֹתוֹת | kwa-vifungo-vya | H5688 |
| אַהֲבָה | upendo | H0160 |
| וָאֶהְיֶה | na-nilikuwa | H1961 |
| לָהֶם | kwao | |
| כִּמְרִימֵי | kama-wanaoondoa | |
| עֹל | nira | H5923 |
| עַל | kutoka | |
| לְחֵיהֶם | shingo-zao | H3895 |
| וְאַט | na-kwa-upole | H5186 |
| אֵלָיו | kwake | H0413 |
| אוֹכִיל׃ | niliwalisha | H0398 |

Niliwaongoza kwa kamba za huruma ya kibinadamu, kwa vifungo vya upendo; niliondoa nira shingoni mwao nami nikainama kuwalisha.

5

| Hebrew | Swahili | Strong's |
|---|---|---|
| לֹא | hata | H3808 |
| יָשׁוּב | rudi | H7725 |
| אֶל־ | kwa- | H0413 |
| אֶרֶץ | nchi-ya | H0776 |
| מִצְרַיִם | Misri | H4714 |
| וְאַשּׁוּר | na-Ashuru | H0804 |
| הוּא | yeye | H1931 |
| מַלְכּוֹ | mfalme-wake | H4428 |
| כִּי | kwa-sababu | |
| מֵאֲנוּ | walikataa | H3985 |
| לָשׁוּב׃ | kurudi | H7725 |

“Je, hawatarudi Misri, nayo Ashuru haitawatawala kwa sababu wamekataa kutubu?

6
וְחָלָה na–utazunguka
חֶ֫רֶב upanga H2719
בְּעָרָיו katika–miji–yake
וְכִלְּתָה na–utamaliza H3615
בַדָּיו makomeo–yake H0905
וְאָכָלָה na–utakula H0398
מִמֹּעֲצֽוֹתֵיהֶֽם׃ kwa–sababu–ya–mipango–yao H4156

> Panga zitametameta katika miji yao, zitaharibu makomeo ya malango yao na kukomesha mipango yao.

7
וְעַמִּי na–watu–wangu
תְלוּאִים wamening'inia H8511
לִמְשׁוּבָתִי kwa–kurudi–nyuma–kwangu H4878
וְאֶל־ na–kwa– H0413
עַל juu H5920
יִקְרָאֻהוּ wananiita H7121
יַחַד pamoja
לֹא hawata H3808
יְרוֹמֵֽם׃ mwinua

> Watu wangu wamedhamiria kuniacha. Hata kama wakimwita Yeye Aliye Juu Sana, kwa vyovyote hatawainua.

8
אֵיךְ nitawezaje
אֶתֶּנְךָ kukuacha H5414
אֶפְרַיִם Efraimu H0669
אֲמַגֶּנְךָ kukusalimisha H4042
יִשְׂרָאֵל Israeli H3478
אֵיךְ nitawezaje
אֶתֶּנְךָ kukufanya H5414
כְאַדְמָה kama–Adma H0126
אֲשִׂימְךָ kukuweka
כִּצְבֹאיִם kama–Seboimu H6636
נֶהְפַּךְ umegeuka H2015
עָלַי ndani–yangu
לִבִּי moyo–wangu
יַחַד pamoja
נִכְמְרוּ zinawaka H3648
נִחוּמָֽי׃ huruma–zangu H5150

> “Efraimu, ninawezaje kukuacha? Ee Israeli, ninawezaje kukutoa? Nitawezaje kukutendea kama Adma? Nitawezaje kukufanya kama Seboimu? Moyo wangu umegeuka ndani yangu, huruma zangu zote zimeamshwa.

9
לֹא sita H3808
אֶעֱשֶׂה tekeleza
חֲרוֹן ukali–wa H2740
אַפִּי hasira–yangu H0639
לֹא sita H3808
אָשׁוּב rudi H7725
לְשַׁחֵת kumwangamiza H7843
אֶפְרָיִם Efraimu H0669
כִּי kwa–sababu
אֵל Mungu H0410
אָנֹכִי mimi H0595
וְלֹא־ na–si– H3808
אִישׁ mtu H0376
בְּקִרְבְּךָ katikati–yako H7130
קָדוֹשׁ Mtakatifu H6918
וְלֹא na–sita H3808
אָבוֹא kuja H0935
בְּעִֽיר׃ kwa–ghadhabu

> Sitatimiza hasira yangu kali, wala sitageuka na kumharibu Efraimu. Kwa kuwa mimi ndimi Mungu, wala si mwanadamu, Aliye Mtakatifu miongoni mwenu. Sitakuja kwa ghadhabu.

10
אַחֲרֵי nyuma–ya
יְהוָה Yahwe H3068
יֵלְכוּ watatembea H3212
כְּאַרְיֵה kama–simba
יִשְׁאָג atanguruma H7580
כִּי־ kwa–sababu–
הוּא yeye H1931
יִשְׁאַג atanguruma H7580
וְיֶחֶרְדוּ na–watatetemeka H2729
בָנִים watoto
מִיָּֽם׃ kutoka–magharibi H3220

> Watamfuata Bwana; atanguruma kama simba. Wakati angurumapo, watoto wake watakuja wakitetemeka kutoka magharibi.

11

| אַשּׁ֑וּר | מֵאֶ֣רֶץ | וּכְיוֹנָ֖ה | מִמִּצְרַ֔יִם | כְצִפּוֹר֙ | יֶחֶרְד֤וּ |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| Ashuru | kutoka–nchi–ya | na–kama–njiwa | kutoka–Misri | kama–ndege | watatetemeka |
| H0804 | H0776 | H3123 | H4714 | H6833 | H2729 |

| ס | יְהוָֽה׃ | נְאֻם־ | בָּתֵּיהֶ֖ם | עַל־ | וְהוֹשַׁבְתִּ֥ים |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| — | Yahwe | asema– | nyumba–zao | katika– | na–nitawarudisha |
| | H3068 | H5002 | | | H3427 |

> Watakuja wakitetemeka kama ndege wakitoka Misri, kama hua wakitoka Ashuru. Nitawakalisha katika nyumba zao,” asema Bwana.

12

| וִֽיהוּדָ֗ה | יִשְׂרָאֵ֑ל | בֵּ֣ית | וּבְמִרְמָ֖ה | אֶפְרַ֔יִם | בְכַ֙חַשׁ֙ | סְבָבֻ֤נִי |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| na–Yuda | Israeli | nyumba–ya | na–kwa–udanganyifu | Efraimu | kwa–uongo | wamenizunguka |
| H3063 | H3478 | | H4820 | H0669 | H3585 | H5437 |

| נֶאֱמָֽן׃ | קְדוֹשִׁ֖ים | וְעִם־ | אֵ֔ל | עִם־ | רָד֙ | עֹ֥ד |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| aminifu | watakatifu | na–na– | Mungu | na– | anatembea | bado |
| H0539 | H6918 | | H0410 | | H7300 | H5750 |

> Efraimu amenizunguka kwa uongo, nyumba ya Israeli kwa udanganyifu. Naye Yuda ni mkaidi dhidi ya Mungu, hata kinyume cha yule mwaminifu Aliye Mtakatifu.